# Tuanze na mazao ya uvuvi kuliteka soko China

Na Scholastica Mazula

SEKTA ya Uvuvi Tanzania inafanyika zaidi katika maziwa na mito kwa asilimia 83 ambapo Ziwa Victoria ndilo linaloongoza kwa uvuvi likifuatiwa na Tanganyika pamoja na Nyasa.

Eneo lote la uvuvi katika maziwa hayo ni takribani kilomita za mraba 50,000. Hata hivyo, uzalishaji wa samaki kwa upande wa baharini ni asilimia 14, na ufugaji asilimia 12.5.

Maeneo ya mito na mabwawa ni Mtera na Nyumba ya Mungu, huku mito mikubwa ambako kunafanyika shughuli za uvuvi ikiwa ni Pangani, Wami, Ruvu, Rufiji na Ruvuma.

Kwa upande wa bahari bado Tanzania haijafanikiwa kuvuna kiasi cha kutosha, kwamba pamoja na kuwa na ukanda mrefu wa bahari wa zaidi ya kilomita 1,400, bado uvuvi katika Bahari ya Hindi unafanyika kwa kiasi kidogo kwani ukanda huo unachangia kati ya asilimia 10 hadi 15 ya shughuli za uvuvi.

Utafiti uliofanywa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kwa kushirikiana na East Africa Trade and Investment hub mwaka 2019, unaonesha kuwa kwa takribani muongo mmoja, uzalishaji wa samaki ulikuwa kati ya tani laki 325 mpaka laki 380. Hata hivyo, kwa makadirio ya mwaka 2021 mahitaji ya samaki nchini ni tani 750,000 kwa mwaka.

Hadi kufikia mwaka 2018, Watanzania waliokuwa wamejiari katika sekta ya uvuvi walikuwa takribani 183,800 ambayo ni sawa na asilimia 0.7 ya nguvu kazi yote nchini, ambapo sehemu kubwa inajihusisha na biashara pamoja na uchakataji.

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) limeziorodhesha nchi ambazo zinafanya vizuri katika eneo la uvuvi barani Afrika na ukiangalia kwenye orodha yake kwa upande wa ukanda wa Afrika Mashariki nchi ambayo ipo kwenye kumi bora kwa maana inayofanya vizuri ni Uganda ikishika nafasi ya sita katika orodha hiyo, wakati Tanzania inashika nafasi ya 11 mbele ya Kenya ambayo iko nafasi ya 18 na nchi inayoongoza kwa uvuvi ni Misri.

Hii inaonesha bado tunahitaji kuongeza juhudi ili kufikia ushindani siyo tu wa kidunia bali Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.

Wakati napitia orodha hiyo, nikakumbuka kuwa kwa sasa wazalishaji wa mazao ya uvuvi wamepata neema kubwa ya soko la bidhaa hiyo huko nchini China, fursa ambayo wameipata kufuatia ziara ya Novembe 2, mwaka huu, iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kufuatia mwaliko wa rais wa nchi hiyo Xi Jinping.



Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki akisisitiza jambo.

> *Hii inaonesha bado tunahitaji kuongeza juhudi ili kufikia ushindani siyo tu wa kidunia bali Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.*

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao walishuhudia utiaji saini wa mikataba na hati za makubaliano ya kimkakati 15 iliyolenga kuimarisha ushirikiano, biashara na uwekezaji baina ya nchi hizo mbili.

China inaongoza kwa uwekezaji nchini Tanzania, ambapo hadi kufikia Oktoba 2022, jumla ya miradi 1,098 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 9.6 ilisajiliwa katika TIC na uwekezaji huo umefanyika katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo na uvuvi.

Kimsingi huu ni uwekezaji wenye tija kwa Taifa letu. Lakini narejea kwenye fursa ambayo hivi karibuni Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki aliitangaza na kuwataka Watanzania wanaojihusisha na bidhaa za uvuvi ikiwemo samaki na mabondo kutumia fursa ya soko kubwa la samaki duniani lililopo China.

Balozi Mbelwa anasema kuwa hiyo ni bahati kubwa kwa wavuvi nchini, lakini swali linalokuja ni je tumejiandaa?

Kiongozi wa Vyama vya Wavuvi Mkoa wa Kigoma ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Wavuvi Tanzania, Francis John anasema anaiona fursa hiyo na anatoa mwito kwa wenzake kuichangamkia.

Mratibu wa Mradi wa Fish YCP na Mfanyakazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa upande wa Tanzania, Hashi Muumini anasema kuwa mradi huo unaangazia kuimarisha mnyororo wa thamani wa uvuvi wa samaki wa Ziwa Tanganyika wakiwemo dagaa wa Kigoma na samaki aina ya Migebuka.


Tafiti za kisayansi zinaonesha kwamba matumizi ya samaki kama chakula inachangia asilimia 30 ya Protini, hivyo ni chakula muhimu kwa afya ya binadamu, wakati wastani wa matumizi ya samaki kwa binadamu ni kilo 20 duniani, kwa Tanzania bado wastani upo chini kiasi cha kilo saba mpaka nane kwa mtu mmoja, hata hivyo ni kiasi kidogo ukilinganisha na wastani wa dunia.

Hata hivyo, Balozi Mbelwa akizungumzia suala la lishe anasema kwamba watakaoruhusiwa kuuza bidhaa hizo nchini China ni Watanzania wenye kampuni zenye miundombinu ya kuvua, kuchakata na kuhifadhi bidhaa za uvuvi wakiwemo samaki na kwamba kampuni hizo zinatakiwa zisajiliwe na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Anasema kuwa ili kila mvuvi, au mchakataji wa mazao ya uvuvi aweze kunufaika, balozi huyo anasema kuwa wananchi wanaojihusisha na shughuli za uvuvi, lakini wanapenda pia kutumia fursa ya soko jipya la kuuza bidhaa za samaki na uvuvi nchini China wasio na kampuni, wanatakiwa baada ya kuvua bidhaa hizo waziuze bidhaa zao kwa wenye kampuni zilizosajiliwa, ambazo zitakuwa na uwezo na ruhusa ya kuuza bidhaa hizo kwenye soko la China.å

Waswahili wanasema ukitaka kujua utamu wa ngoma ingia ucheze. Nam, utamu na mafanikio ya wavuvi wanaujua wenyewe maana ndiyo wanaoicheza ngoma, wafanyabiashara wa samaki jijini Mwanza mbali na kuishukuru Serikali kwa kuendelea kufungua milango ya fursa, wanaiomba pia kupitia Wizara yenye dhamana iwekeze kwenye elimu ili wavuvi, wachakataji na wadau wa samaki kwa ujumla waweze kuitumia na kunufaika na fursa hiyo.

***Mwandishi wa makala haya ni Mhariri Mkuu wa Redio ya EFM na TV E.***



Mvuvi akitoka ziwani kuvua samaki.